

HALMASHAURI YA MJI TARIME

TAREHE 21 Aprili, 2022

TANGAZO LA KAZI YA UWEKAJI MIUNDOMBINU YA MAJI, UMEME, MILANGO NA MADIRISHA YA ALUMINIUM, UMALIZIAJI (RIPU, SAKAFU, DARI, MAPAMBO) KATIKA JENGO LA UTAWALA HALMASHAURI YA MJI TARIME (Kuongeza Muda wa Kuomba)

1. Mkurugenzi wa Mji Tarime anapenda kuwatangazia watanzania wote wenye ujuzi na sifa za kujenga majengo ya Serikali kuleta maombi ya kazi ya Ukamilishaji ujenzi katika jengo la Utawala.

2. Sifa ya mwombaji

i. Awe na Ujuzi wa Ufundi wa Kazi husika.

ii. Awe mtanzania. Aambatishe nakala ya kitambulisho cha Taifa/Mpiga kura

iii. Awe na uzoefu wa kazi hii usiopungua Miaka 3. Aambatishe nakala ya mkataba au nyaraka za kazi alizowahi kufanya.

iv. Awe na ujuzi wa kusoma na kutafsiri michoro/Ramani ya Majengo.

v. Awe na uwezo wa kupata mafundi wasaidizi /vibarua na kuwalipa mwenyewe kabla hajalipwa na Halmashauri kwa kazi husika.

vi. Awe mwaminifu. Awe tayari kuwajibika kwa upotevu wa vifaa vya ujenzi alivyokabidhiwa eneo la ujenzi.

vii. Awe na TIN Namba.

3. Barua ya maombi iandikwe kwa mkono, ipitie kwa mwenyekiti wa mtaa/kijiji/kitongoji anakoishi ikiwa na wasifu (CV) ya uzoefu wa kazi za ujenzi wa majengo ya serikali au taasisi ulizowahi kufanya.

4. Kwa maelekezo na ufafanuzi wa kazi uliza kupitia barua pepe: td@tarimetc.go.tz

5. Maombi yote yatumwe kwa Mkurugenzi wa Mji, S.L.P 45 TARIME.

6. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 27 Aprili, 2022 saa Tano kamili Asubuhi.

NB: ADA YA MAOMBI NI TZS 10,000 (ELFU KUMI TU) NA HAIRUDISHWI



Gimbana E. Ntavyo

MKURUGENZI WA MJI TARIME

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA MJI WA
TARIME